# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)
# HALMASHAURI YA MANISPAA IRINGA

**Anuani ya Simu:**
**Iringa,**
**Simu Na 0625994165/**
**0737928020/0754377577**

**Shule ya Wasichana**
**S. L. Pekee,**
**IRINGA.**

**Kumb,Na IGS/J/5/2023**

**15/12/2023**

Ndugu,
Mzazi / Mlezi wa
________________________________
________________________________

## YAH:- MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA IRINGA, HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA MWAKA 2024

**1.0: UTANGULIZI.**
Nafurahi kukutarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha Kwanza (I) katika shule hii mwaka **2024.** Shule ya Sekondari ya Wasichana Iringa ipo umbali wa **km 13** kutoka stendi kuu ya mabasi Iringa, kando kando ya barabara kuu iendayo Dodoma. Usafiri daladala kutoka stendi kuu hadi stendi kuu ya zamani ni shilingi **700/=** na kutoka stendi kuu ya zamani hadi shuleni ni shilingi **700/=** na kwa usafiri wa taxi ni shilingi **20,000/=** kutoka stendi kuu hadi shuleni. Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **08/01/2024** unatakiwa kuripoti shuleni kabla ya saa kumi jioni, mwisho wa kuripoti ni tarehe **15/01/2024** yaani ndani ya siku saba.

**1.1: MOTTO WA SHULE:**
"**JUHUDI NA MAARIFA HULETA USHINDI" (Struggle for success)**
Hii ndio kauli mbiu (Motto wa shule). Ni matumaini yangu utaitakafari na utaitumia nafasi hii Kwa manufaa yako, jamii na taifa kwa ujumla.

**2.0: MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.**

**2.1: Sare za Shule.**

**i. Sare za kawaida.**

a) Sketi mbili zenye marinda rangi ya orange ndefu hadi funda la chini la mguu.
b) Shamba sketi mbili zenye marinda dark blue ndefu hadi funda la chini la mguu.
c) Tracksuit mbili rangi Blue Bahari (bluu ya kupauka) yenye miraba myeupe miwili au mitatu na isiyo na kofia.
d) Sweta mbili rangi ya damu ya mzee (Maruni).
e) Shati nyeupe mikono mifupi mbili.
f) T-Shirt rangi dark blue mbili zenye kola.

**ii. Sare ya Hijabu.**

a) Sketi mbili za marinda orange ndefu zinazofika funda la chini la Mguu.
b) Shati mbili ndefu za mikono mirefu (nusu kanzu) nyeupe.
c) Vitambaa vya kichwani (Hijab) viwili visivyo na mapambo yoyote vyeupe.
d) Sketi mbili zenye marinda dark bluu ndefu hadi chini.
e) T-shirt rangi dark blue mbili zenye kola.

**iii. Sare nyingine.**

a) Soksi nyeupe ndefu jozi nne.
b) Raba nyeupe pea mbili (zisizo na mchanganyiko wa rangi yoyote) za kamba zisizo na kisigino kirefu) kwa ajili ya kuvaa darasani.
c) Raba nyeusi pea moja (zinavaliwa baada ya kutoka darasani) zenye kamba.
d) Jezi ya Yanga (Rangi ya Kijani) kwa ajili ya michezo.
e) Pullneck nyeupe

**2.2 Mahitaji Mengine muhimu kwa matumizi binafsi ya mwanafunzi.**

a. Godoro la futi 2.5
b. Blanketi 1
c. Mto 1
d. Shuka za pinki 2 na foronya 2
e. Ndoo ya kuogea ya lita 10 moja (Green).
f. Picha za wazazi au walezi (Passport size) kwa kila mzazi/mlezi na mwanafunzi (mbili) zibandikwe kwenye fomu iliyoambatishwa
g. Chandarua nyeupe futi 3
h. Sabuni ya maji lita 5 ya kufanyia usafi.
i. Sabuni ya unga kilo 10 na fagio ngumu(hard broom).
j. Vyombo vya chakula sahani, bakuli, kikombe, kijiko.
k. Nguo za ndani za kutosha
l. Kandambili za kuogea. (siyo yeboyebo).
m. Taulo 1, Toilet paper 5, taulo za kike (Pads) si chini ya paketi 5
n. Kanga jozi mbili kwa Muislamu na jozi moja kwa Mkristo
o. Vifaa vya masomo (taaluma) **(i)** Madaftari makubwa (counter books quare four, 14), **(ii)** Kamusi ya kiingereza - kiswahili, **(iii)** Kamusi ya kiingereza - kiingereza **(iv)** kalamu za wino za kutosha bluu au nyeusi, kalamu za risasi, **(v)** rula cm 30 **(vi)** vifutio na vichongeo, Ream 1 ya karatasi A.4, (kwa mwaka), Begi la kubebea madaftari na Mathematical set.
p. Sabuni za kufulia na kuogea (medicated soap) za kutosha
q. Fedha za kutosha za matumizi binafsi ya mwanafunzi
r. Faili (**flat Plastic file**) dogo la kutunza kumbukumbu za mwanafunzi 1.
**s. Ni lazima mwanafunzi akaja na kadi ya bima ya afya au aje na tsh. 50,400/= kwa ajili ya bima ya afya kwa matibabu ya mwaka mzima (NHIF). kadi ya bima afya itakaguliwa au pesa itapokelewa siku ya kuripoti.**
t. Ni vema mzazi ukahakikisha mtoto anapokuja shuleni awe amechukua **tahadhari zote za kiafya.**
u. Blanket na Trunker (sanduku la chuma).
v. Ndoo moja lita ishirini kwa matumizi ya shule.
w. Saa ya mkononi isiyo ya mshale (kwa ajili ya kutunza muda) kwa matumizi yake binafsi.
x. Rim za karatasi A4 mbili, moja kwa kila muhula.

**2.3: Uhuru wa Kuabudu.**

Utaruhusiwa kuabudu kwa kufuata sheria, ratiba na taratibu za shule na za nchi.

**2:4: Kubadili Dini.**

**Hutaruhusiwa** kubadili dini, ukiwa shuleni.

**2.5: Kubadili jina.**

Hautaruhusiwa kubadili jina. Jina lako linatakiwa kuwa kama ilivyotumika wakati wa mitihani wa darasa la Saba na kwenye **TSM9 FORM** yako. Ili kupunguza usumbufu wa usajili kutoka kipengele hiki, mwanafunzi anaporipoti shuleni, anatakiwa kuja na nakala (**Photocopy**) ya cheti chake cha kuzaliwa. Hii itasaidia kuepuka matatizo yanayoweza kujitokeza wakati wa usajili wa mtihani wa taifa.

**2.6: Kuwatembelea wanafunzi/siku ya wageni shuleni.**

Wazazi/walezi wataruhusiwa kuwatembelea wanafunzi mara moja kwa muhula kwa tarehe itakayopangwa itakuwa siku ya Jumapili kuanzia saa 4.00 asubuhi mpaka 10.00 jioni. Mwalimu wa darasa atakuwepo kuonana na wazazi ili kujadiliana kuhusu maswala ya kitaaluma na nidhamu ya mwanafunzi. Hairuhusiwi kumletea mwanafunzi aina yoyote ya chakula. Aidha, mawasiliano mengine muhimu yapitie kwa mkuu wa shule kwa anuani iliyopo hapo juu au simu Namba **0625994165/0758453468/0737928020.**

**N.B:- Hairuhusiwi mwanafunzi kumiliki simu, line, au chaja akiwa shuleni wala kuletewa na mzazi siku anapotembelewa shuleni, ikibainika hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa.**

**2.7: Mpango wa Usafiri.**

Mpango wa Usafiri. Unapokuja na kurudi nyumbani wakati wa likizo utajilipia nauli. Usafiri wakufika Iringa ni kwa njia ya mabasi. Mwalimu wa usafiri atakusaidia kufanya mpango wa usafiri wakati wa kwenda na kurudi likizo. Mzazi unatakiwa kumlipia mtoto wako nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani mapema, ili mipango ya usafiri ifanyike mapema. Ni lazima mwanafunzi asafiri akiwa amevaa sare ya shule kila anapokwenda nyumbani na kurudi shuleni

**2.8: Vitu visivyoruhusiwa shuleni.**

a) Simu za mkononi (charger, line za simu, vocha na vyote vinavyoendana na simu) Mawasiliano muhimu baina ya mzazi/Mlezi na mwanafunzi yafanyike kupitia kwa Mkuu wa Shule kwa anuani tajwa hapo juu.
b) Pasi za umeme, heater, birika la umeme
c) Kusuka nywele au kuweka dawa za aina yoyote ile
d) Kupaka rangi kucha au kupaka ina, wanja na lipstic
e) Nguo za nyumbani zisizo sare ya shule.
f) Heleni, Mkufu, pete na bangili.

**3.0: Sheria na Kanuni muhimu za shule.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, sayansi, teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu chini ya ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleini.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni na asubuhi (preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shuleni na nyingine utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa wanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule

g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
i) Kutunza mali za umma
j) Mwanafunzi anatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote awapo shuleni.

**3.1: Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha KUFUKUZWA** au **KUSIMAMISHWA** shule

(a) Wizi.
(b) Utoro
(c) Uasherati na ushoga.
(d) Ubakaji.
(e) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
(f) Kupigana na kupiga.
(g) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
(h) Kudharau Bendera ya Taifa.
(i) Kuwa mjamzito/kupata mimba.
(j) Kutoa mimba.
(k) Kuoa au kuolewa.
(l) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu.
(m) Kukataa adhabu kwa makusudi.
(n) Kuwa na simu ya mkononi.

**4.0: Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.**

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wakutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

**5.0:** Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA IRINGA**

**NGATUMBURA L. H**
**MKUU WA SHULE**
**SIMU; 0625994165/0758453468**

HEADMISTRESS
IRINGA GIRLS SECONDARY SCHOOL
PRIVATE BAG
IRINGA

**Nakala kwa:-** **- Katibu Mkuu, - Tamisemi**
**- Mkurugenzi Manispaa, IRINGA**

**6.1: (a) MEDICAL EXAMINATION.**

## PRESIDENT'S OFFICE, REGIONAL ADMINSTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
## IRINGA MUNICIPAL COUNCIL

Tel. No
School,
0282702555

Iringa Girls Sec
Private Bag,
**IRINGA.**

**Ref. No IGS/MED/VOL.I/2023**

____________________

To The Medical Officer,
_________________________
_________________________
_________________________

**REF:- REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF______________________________ STUDENT**

Please examine the above named student for her fitness to pursue her advanced secondary eduction.

i. Age/ Years ____________________________________________________________________
ii. Blood found (red and White)_____________________________________________________
iii. Stool examination______________________________________________________________
iv. Urinalysis ____________________________________________________________________
v. Venereal Diseases test__________________________________________________________
vi. T.B. test______________________________________________________________________
vii. Eye Test_____________________________________________________________________
viii. Ears_______________________________________________________________________
ix. Abdomen_____________________________________________________________________
x. Chest_________________________________________________________________________
xi. Spleen_______________________________________________________________________
xii. Urine for Pregnant ____________________________________________________________

**ADDITIONAL INFORMATION** (If any) e.g. Physical defects, impairment(s) e.g. arm, leg etc. infection chronic or family disease etc___________________________________________________
__________________________________________________________________________________
____________________________________________________________________________

__________________ __________________

___________________

**Date** **Designation** **Sig and Official stamp**

**Fomu hii ijazwe kikamilifu na daktari na mwanafunzi aje nayo siku ya kuripoti shuleni.**

## 6.1: (b) TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI:

1. Jina kamili la mwanafunzi ________________________________________
   Mahali alipozaliwa ________________________________________
   Tarehe ya Kuzaliwa____________________Umri ____________________
   Anuani ya nyumbani ________________________________________
   Shule ya sekondari aliyosoma________________________________________
   Namba ya mtihani Darasa la saba____________________________________
   Kabila__________________________Dhehebu_______________________

**PICHA YA MWANAFUNZI**

2. Jina kamili la Baba ________________________________________
   Kabila ____________________ Dhehebu _____________________
   Simu Na___________________ Kazi_________________________

**PICHA YA BABA**

3. Jina kamili la mama ________________________________________
   Kabila ____________________ Dhehebu ______________________
   Simu Na __________________ Kazi __________________________

**PICHA YA MAMA**

4. Jina kamili la Mlezi ________________________________________
   Kabila ____________________ Dhehebu ______________________
   Simu Na __________________ Kazi __________________________

**PICHA YA MLEZI**

**(Unaeishi Nae)**

5. Je, wewe unaishi na nani? Jina
   ________________________________________________
   Uhusiano
   ________________________________________________________________
   Anuani
   ____________________________________________________________________

6. Je, uliwahi kuwa kiongozi?
   Ndiyo/Hapana________________________________________
   Kama ndiyo taja nafasi ilikuwa ipi? ____________________________________________
   ________________________________________________________________________

7. Utakuwa unakwenda wapi wakati wa likizo________________________________________
   (Wakati wa likizo unatakiwa kwenda kwa mzazi au mlezi aliyetajwa tu. Kama utabadilisha mahali pa kwenda likizo, mzazi/mlezi atoe idhini kwa maandishi mwezi mmoja kabla)

## 6:1 (c) AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi (Jina kamili)___________________________________________________________

Anuani
_______________________________________________________________________

Simu _______________________________________________________________________

Mzazi/Mlezi _________________________________________________________________

Nakubali mtoto wangu (Jina lake) _____________________________________________

1. Asome katika shule ya Sekondari ya Wasichana Iringa, kadiri alivyopangiwa.
2. Nimempa fedha ya mahitaji inayotakiwa na nitashirikiana na walimu katika suala zima la malezi ya mwanangu na maendeleo yake kitaaluma na kumsaidia mtoto kufuata sheria za shule.

Jina (Mzazi/Mlezi)___________________________________________________________

Saini ______________________________________________________________________

Tarehe_____________________________________________________________________

Namba ya simu______________________________________________________________

Namba ya simu yenye **WhatsApp** ya kwako au miongoni mwa ndugu wa Mwanafunzi walioonyeshwa kwenye Form hii au unaweza kutuma ujumbe wa kuomba kuunganishwa kwenye Group la Wazazi kwenda namba **+255 753 243 401** (**ni Muhimu**)____________________

Mimi (Jina la Mwanafunzi)_______________________________________________________

Nimekubali nafasi hii, naahidi kufuata sheria za shule na kuwatii walezi na wakubwa, tena nitafanya bidii ya kujifunza ili nifaulu vyema masomo yangu.

Jina _______________________________________________________________________

Saini ______________________________________________________________________

Tarehe_____________________________________________________________________